

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
7 Juni 2008**

Mahudhurio

Ally Athuman Jumbe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Markus Weise

Ofisi

Wakati wa wiki Juma alilipa kodi ya Tsh 240,000 kwa ajili ya mwaka 1 / 8 / 2008 mpaka 1 / 8 / 2009 kwa Juma Hassan Chibaya, mwenye ofisi ya Manzese. Walisaini mkataba. Wakati wa wiki Juma Hassan Chibaya alichangia muda wake kwa kupaka rangi ndani na nje ya ofisi Manzese kwa kutumia rangi iliyobaki kutoka ofisi ya Mabibo. Mejah alimwambia Elaine kwamba atapaka rangi ya nembo na jina letu. Ally Athman alipendekeza tuandae tangazo kuweka ofisini Mabibo kusema tumehamia Manzese Argentina Mtaa wa Sisi kwa Sisi karibu na Mid Land Bar. Juma alinunua kifunguo kwa ajili ya ofisi mpya – yeye ana ufunguo mmoja, Elaine ana nyingine na Juma Chibaya ana nyingine.

Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund

Jumatano Juma na Markus walitembelea HUWATA. HUWATA walisema wataandaa repoti kuhusu shule walizotembelea. Pia watakodi baisikeli na wataenda pamoja na Juma na Markus mpaka Kigamboni wiki ijayo. Walikuwa na wazo kuandika barua kwenda kwa magazeti kuwapa taarifa ya mradi wetu. Wanachama wa UWABA walikubali kwamba ni wazo mzuri ila watupe nakala kwanza tupitie. Waliomba Juma anunue kitabu cha vocha kwa UWABA kwa ajili ya utawala.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Mbondole alimpigia simu Elaine kusema watapenda sana kushirikiana katika mradi. Elaine alisema atawasiliana nao tena kualika mwalimu mmoja kwenye training of trainers.

Markus alitumia credit card yake kulipa ndege ya Andrew kwenda Dar es Salaam, na Elaine na Juma walichukua hela kutoka akaunti ya UWABA kurudisha hela zake. Gharma ilikuwa Tsh 974,000 ambayo ni juu kidogo kulika badjeti yetu.

Andrew alisema kwa email kwamba bado anatengeneza karatasi za mafunzo na atatutumia baada ya wiki chache.

NIT walisema kwa email kwamba wamefanya booking ya darasa kwa ajili ya wiki ile.

TANROADS na barabara mpya

Markus ataprint picha za barabara mpya na ataenda TANROADS wiki ijayo.

Kodi

Ally Athman alitukumbusha tutafute taarifa kuhusu kodi ya baisikeli kuingia nchini.

Siku ya Mazingira

Juma alisikia tangazo ya sherehe ya siku la mazingira Mnazi Mmoja na alienda na Markus alhamisi. Walisambaza vipeperushi vilivyobaki kutoka msafara wa baisikeli.

Mambo ya hela

Juma alitumia Tsh 2,000 kwa ajili ya kifunguo na Tsh 1,000 kwa ajili ya fundi kurekebisha mlango wa ofisi Manzese. Kodi ya Tsh 240,000 ililipwa na Tsh 200,000 kutoka benki na Tsh 40,000 ya hela ya UWABA ambayo Juma anayo nyumbani. Juma sasa ana Tsh 46,500 ya hela ya UWABA nyumbani.